



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MJI NZEGA**



Unapojibu tafadhali taja

Kumb.Na. NTC/CA4/2/80

TAREHE 24/08/2021

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Nzega amepokea Kibali cha Ajira Mbadala chenye **Kumb.Na FA.170/365/01/"B"/130** cha tarehe **22 Julai, 2021** kutoka kwa **Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora**. Katika Nafasi zifuatazo:

- 1. Mtendaji wa Mtaa Daraja la III – Nafasi 01**
- 2. Dereva Daraja la II - Nafasi 01**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Nzega anakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa Watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi hizo kama ilivyo ainishwa katika Tangazo.

MTENDAJI WA MTAA III - TGS B (NAFASI 01).

1.0 MTENDAJI WA MTAA DARAJA LA III – (NAFASI 01)

SIFA ZA MWOMBAJI

Awe na Elimu ya Kidato cha nne (IV) au Kidato cha sita (VI), aliyehitimu mafunzo ya cheti/Astahada (**Cheti cha NTA LEVEL 5**) katika moja ya fani zifuatazo: Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo - Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

MAJUKUMU YA KAZI.

- i. Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Mtaa
- ii. Kusimamia Ulinzi na Usalama wa Raia na Mali zao, kuwa Mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Mtaa
- iii. Kuratibu na kusimamia upangaji na utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Mtaa
- iv. Kuratibu Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Mtaa
- v. Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu
- vi. Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha Wananchi katika kuandaa na kutekeleza Mikakati ya kuondoa Njaa, Umasikini na kuongeza uzalishaji mali

2.0 DEREVA DARAJA LA II – TGS B (NAFASI 01)

SIFA ZA MWOMBAJI.

Awe na cheti cha Kidato cha nne (IV) na Leseni ya Daraja la E au C1 ya uendeshaji magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua Mwaka mmoja bila kusababisha ajali.

Awe amehudhuria mafunzo ya Msingi ya uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) au Chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali

KAZI NA MAJUKUMU

- i. Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari
- ii. Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi
- iii. Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari
- iv. Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali
- v. Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari
- vi. Kufanya usafi wa gari
- vii. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na Msimamizi wake wa kazi

MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI.

- i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri kuanzia miaka 18 na usiozidi miaka 45
- ii. Waombaji wote waambatanishe cheti cha kuzaliwa.
- iii. Waombaji waambatanishe maelezo binafsi (WASIFU) yanayojitosheleza (Detailed CV) yenye anwani na namba za simu zinazopatikana pamoja na majina ya Wadhamini (Referees) watatu wa kuaminika.
- iv. Maombi yote yaambatane na vyeti vya Elimu na Taaluma yaani nakala ya cheti cha kidato cha nne au sita, Vyeti vya Taaluma na picha mbili za rangi za hivi karibuni
- v. Waombaji wote wanalazimika kuwa na **Namba ya Utambulisho wa Uraia** (National Identification Number) kutoka Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA)
- vi. Testimonials”, “Provisional Results;”, “Statement of Results”. Hati ya matokeo ya kidato cha nne na sita, yaani **FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS HAVITAKUBALIWA.**
- vii. Waombaji wa Nafasi za Ajira waliostafishwa kazi, Waliofukuzwa kazi, na kuachishwa kazi katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana Kibali kutoka kwa **Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.**
- viii. Uwasilishaji wa Taarifa na sifa za kugushi, waombaji **watachukuliwa** hatua za kisheria
- ix. Mwisho wa kupokea barua za maombi ni **tarehe 06/09/2021** Saa 9:30 Alasiri.
- x. Maombi yote yatumwe kwa njia ya mkono au Posta kupitia Anuani ifuatayo:

MKURUGENZI,

HALMASHAURI YA MJI NZEGA,

S.L.P 256,

NZEGA

IMETOLEWA NA:



Shomary S. Mndolwa,
**MKURUGENZI WA MJI,
NZEGA.**

**MKURUGENZI
HALMASHAURI YA MJI
NZEGA.**